العقيقة

AL-AQIQA

KIMEKUSANYWA NA:

AL-AKH MAHMOUD HUMEID

KIMEPITIWA NA:

SHEIKH ABU HASHIM

NA

ABUL KHATAAB ABDALLAH

Contents

UTANGULIZI 1

UTANGULIZI WA MUANDISHI 1

AQIQA: 2

MAANA YA AQIQA..... 2

HUKMU YA AQIQA 2

MAANA YA KUWEKWA REHANI 4

WAKATI WA AQIQA..... 4

YULE AMBAE HAKUCHINJIWA AQIQA NA WAZAZI WAKE 6

AKIFA MTOTO KABLA SIKU YA SABA 6

KIWANGO CHA AQIQA 7

HUKMU YA KUCHINJA MNYAMA MWENGINE MBALI NA MBUZI AU KONDOO 8

IPI BORA? KUCHINJA AU KUTOA THAMANI YAKE?? 9

JE KUNA DHIKR [UTAJO] MAALUM WAKATI WA KUCHINJA AQIQA? 10

KUIGAWA NYAMA YA AQIQA..... 11

HUKMU YA KUVUNJA MIFUPA YA MNYAMA WA AQIQA 12

HUKMU YA KUKUSANYA NIYYAT (MBILI) YA AQIQA PAMOJA NA UDH-HIYA 12

JE INASHURUTISHWA KATIKA AQIQA KAMA VILE INAVYOSHURUTISHWA KATIKA UDH'HIYA?..... 13

KUALIKA WATU KWA AJILI YA AQIQA 14

KUKOPA KWA AJILI YA AQIQA..... 14

KUMPA KAFIRI KATIKA NYAMA YA AQIQA..... 15

TOFAUTI BAINA YA UDH'HIYA NA AQIQA 15

KUMPA MTOTO JINA..... 16
WAKATI GANI MTOTO HUPEWA JINA?..... 16
KUMPA MTOTO JINA ZURI..... 17
KUNYOA NYWELE ZA MTOTO..... 18
HUKMU YA KUTOA THAMANI BILA KUNYOA NYWELE WALA KUPIMA..... 19
FAIDA YA KUNYOA NYWELE ZA MTOTO..... 19
KUNYOA NYWELE ZA MTOTO WA KIKE..... 20
HUKMU YA ADHANA NA IQAMA KWENYE SIKIO LA MTOTO..... 20
TAHNIK..... 21

UTANGULIZI

Sifa njema zote ni za Allah Mtukufu na rehma na Amani zimshukie Mtume wetu Muhammad ﷺ na jamaa zake na masahaba wake wote.

Mtume ﷺ ametuwekea Sunna ya Aqiqa (kumchinjia mtoto mbuzi au kondoo) baada ya kuzaliwa mtoto huyo, na ni mbuzi au kondoo mmoja kwa mtoto wa kike na mbuzi au kondoo wawili kwa mtoto wa kiume. Na Aqiqa ni mara moja tu katika umri wa mtoto huyo.Na hii ni katika sunna zilizowachwa na baadhi ya waislamu, kwa sababu ya kufuata utamaduni wa kimagharibi wa kufanya Birthday kwa mtoto ambapo uislamu umeharamisha jambo hilo, kwani ni kujifananisha na makafiri. Na Mtume ﷺ anasema: "**من تشبه بقوم فهو منهم**" Mwenye kujifananisha na watu basi yeye ni katika wao.

Kwa hivyo ni juu ya waislamu kuihuisha sunna hii ya Aqiqa kwa kishindo kikubwa, na kuliuwa jambo hilo la kufanya Birthday, kwani jambo hili limeenea sana kwa waislamu licha ya madhambi wanayoyapata kwa kufanya jambo hilo la kikafiri.

Pengine kitabu hiki kilichoandikwa na ndugu yetu Mahmoud Humeid kitakua ni sababu ya waislamu kuamka na kuitekeleza

sunna hii ya Aqiqa na kupata thawabu kutoka kwa Allah Subhanahu wata'ala.

Tunamuomba Allah aijaalie amali hii ya ndugu yetu katika mizani ya amali zake njema, na amzidishie Baraka katika elimu yake yeye na watoto wake na waislamu wote.

Abu Hashim

22/2/1438 – 22/11/2016

بسم الله الرحمن الرحيم

إِنَّ الْحَمْدَ للهِ، نَحْمَدُهُ، وَنَسْتَعِينُهُ، وَنَسْتَغْفِرُهُ، وَنَعُوذُ بِاللهِ مِنْ شُرُورِ أَنْفُسِنَا، ومِنْ سَيِّئَاتِ أَعْمَالِنَا، مَنْ يَهْدِه

اللهُ فَلاَ مُضِلَّ لَهُ، وَمَنْ يُضْلِلْ فَلاَ هَادِيَ له، وَأَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيكَ لَهُ, وَأَشْهَدُ أَنَّ

مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ صلي الله عليه وعلى آله وسلم.

أَمَّا بَعْدُ:

فإن أصدق الحديث كتاب الله، وخير الهدي هدي محمد صلى الله عليه وعلى آله وسلم, وشر الأمور

محدثاتها, وكل محدثة بدعة, وكل بدعة ضلالة, وكل ضلالة في النار.

UTANGULIZI WA MUANDISHI

Hakika katika sunna zilizo achwa na kugurwa na watu wengi katika zama hizi, ni sunna ya Aqiqa, pamoja na kuwa Mtume ﷺ ameifanya na kuihimiza sunna hii.

Basi yampasa muislamu alitilie umuhimu sana jambo hili haswa wale ambao Allah subhaanahu wataala amewapa wasaa. Na awe na ikhlas katika kutekeleza na kuihuisha sunna hii.

Amesema Sheikh Albany –rahimahullah-:

“Lazima kuwakumbusha jambo [moja] ambalo huenda baadhi ya watu wakawa na haja nalo. Baadhi ya wale wanaoalika watu kwa ajili ya aqiqa, ni wajib wamkusudie Allah subhaanahu wata’ala [ikhlas], wasikusudie nyuma ya hilo umaarufu wala kujionyesha wala kusemwa [kwa vizuri], na zamani walisema baadhi yao: “Kupenda kudhihiri [kuonekana] kunavunja migongo”, bali iwe ni kwa ajili ya Allah alietukuka, na akusudie kuwalisha mafukara, na marafiki, na kuweka majlis ya ilmu kama alivyofanya ndugu yetu hapa, yote hayo makusudio yake ni radhi za Allah alietukuka. Huu ni ukumbusho, na ukumbusho una wanufaisha waumini.”

[Silsilatil Hudaa wa Nnur kaseti nambari (20)].

Katika risala hii ndogo nitataja kwa mukhtasari baadhi ya hukmu zinazofungamana na Aqiqa, nikimuomba Allah subhaanahu wataala aijaalie ni risala iliokusudia radhi zake [peke yake], isiokuwa na riyaa wala lengo lengine lolote la kidunia.

AQIQA:

MAANA YA AQIQA

AQIQA, kilugha: Imetokamana na neno "العق", nako ni kukata.

Na asli yake, ni nywele zinazopatikana katika kichwa cha mtoto aliezaliwa.

Na **kisheria**: Ni mnyama anaechinjwa siku ya saba kwa ajili ya mtoto aliezaliwa, wakati [pia] ananyolewa nywele zake.

[Fiqh al muyassar (1/196)].

HUKMU YA AQIQA

Wametofautiana wanavyuoni juu ya hukmu ya aqiqa kwa qauli tatu.

1. **Wajib**
2. **Sunna Muakkada –** Sunna iliokokotezwa - Nayo ni qauli ya wengi ya wanavyuoni.
3. **Mubah**

Amesema Al-Imam Ibn Baaz –rahimahullah-:

"Aqiqa ni <u>Sunna iliokokotezwa</u> wala sio wajib, mtoto wa kiume [atachinjiwa] mbuzi au kondoo wawili na mtoto wa kike mbuzi au kondoo mmoja….."

[Majmu'u Fatawa (18/50)].

Na dalili inayo onyesha kupendekezwa kwake [kuwa ni Sunna], ni hadith ya Mtume ﷺ aliposema;

“Yule atakaeruzukiwa mtoto, kisha <u>akapenda kumchinjia</u> [aqiqa] basi na amchinjie, kwa mtoto wa kiume mbuzi au kondoo wawili walio sawa na kwa mtoto wa kike mbuzi au kondoo mmoja”

Abu Daud [2842], Hadithi hii ni Hassan kama ilivyo katika Sahih Sunan Abi Daud.

Mtume ﷺ akafungamanisha amri yake na mapenzi ya mwenye kuchinja, na hii ni dalili kwamba ni sunna wala sio wajib.

Tuhfatul Maudud [ukurasa; 157].

Na dalili inayoonyesha kukokotezwa kwa Sunna hii ni hadithi aliyoipokea Bukhari katika sahih yake kutoka kwa Salman bin Amer Adhabby -radhiallahu anhu- asema; Nilimsikia Mtume ﷺ akisema;

“Kila mtoto na aqiqa yake, mchinjieni, na mumuondolee udhia [kwa kumnyoa nywele].”

Na amepokea Samura bin Jundub -radhiallahu anhu- kwamba Mtume ﷺ asema;

“Kila mtoto amewekwa rehani kwa aqiqa yake, atachinjiwa siku ya saba, na ataondolewa udhia [kunyolewa nywele], na atapewa jina.”

Tirmidhi [1522] Ibn Majah [3165] Sahih Ibn Hibban [2563].

MAANA YA KUWEKWA REHANI

Amesema Sheikh Muhammad Bin Swaleh Al-Utheimin –rahimahullah-

“Hakika ya maana yake ni kuwa, amezuiliwa [mtoto yule] kutokamana na kufungukiwa na raha ya nafsi, vile vile [amezuiliwa] kutokamana na kuhifadhiwa na sheitan.”

Sharhul Mumti’i [3/431].

WAKATI WA AQIQA

Ni Sunna aqiqa iwe siku ya saba kutoka kuzaliwa kwa mtoto, kwa hadith iliotangulia ya Samura bin Jundub -radhiallahu anhu-;

“Kila mtoto amewekwa rehani kwa aqiqa yake, atachinjiwa siku ya saba, na ataondolewa udhia [kunyolewa nywele], na atapewa jina.”

Tirmidhi [1522] Ibn Majah [3165] Sahih Ibn Hibban [2563].

Amesema Sheikh Swaleh Al-Fawzan –hafidhahullah-;

“Na lau akichinja kabla ya siku ya saba au baada yake, itafaa.”

Al-Mulakhas Al-Fiqhy [ukurasa; 215].

Na siku ya kuzaliwa kwake pia inahisabiwa kwa qauli sahih ya wanavyuoni na ndio qauli ya Hanaabila na wengineo.

Amesema Sheikh Ibn Utheymin –rahimahullah-;

“Ni Sunna achinjiwe siku ya saba, akizaliwa siku ya Jumamosi – kwa mfano - basi atachinjiwa siku ya Ijumaa, yani siku moja kabla ya ile siku aliozaliwa, hii ndio qaaida, na akizaliwa siku ya Alkhamisi basi atachinjiwa siku ya Jumatano na kadhalika….”

Isipowezekana siku ya saba basi jumhur ya wanavyuoni wanapendekeza siku ya kumi na nne (14), na isipowezekana basi siku ya ishirini na moja (21).

Wakatolea ushahidi maneno ya Mama Aisha –radhiallahu anhaa- asema;

“Na iwe [aqiqa] ni siku ya saba, isipowezekana basi siku ya kumi na nne, na isipowezekana basi siku ya ishirini na moja.”

Ameidhoofisha hadith hii Albany katika Al-Irwaa [4/395-396].

Na Leith na Ibn Siirin wameenda na qaul ya kutozingatiwa isipokuwa wiki ya kwanza peke yake [kwamba ndio Sunna], ama baada ya hapo basi atachinjiwa siku yoyote bila kuzingatia siku maalum.

Aliulizwa Al-Allama Abdul Muhsin Al-Abbad kuhusu Aqiqa siku ya kumi na nne na siku ya ishirini na moja…

Akajibu; **“Wallahy halikuthibiti hilo, yamekuja mapokezi ambayo hayakuthibiti [sio sahih] kwamba inakadiriwa siku ya kumi na nne au ishirini na moja, imepokewa hadithi dhaifu.”**

[Sharh Sunan Abi Daud kaseti nambari (209)].

YULE AMBAE HAKUCHINJIWA AQIQA NA WAZAZI WAKE

Asema Ibn Siirin –rahimahullah-;

“Lau najua kwamba sikuchinjiwa [Aqiqa] basi ningejichinjia nafsi yangu.”

[Silsila Assahiha (6/206)].

Na akasema Al-Hassan Al Basry –rahimahullah- ;

‘Ikiwa hukuchinjiwa Aqiqa basi jichinjie nafsi yako’.

[Silsila Assahiha (6/206)].

AKIFA MTOTO KABLA SIKU YA SABA

Sahih katika mas’ala haya ni kwamba ni sunna mtoto achinjiwe hata kama hakukamilisha siku saba ya uhai wake, kama ilivyokuja katika hadith zilizotangulia;

“Kila <u>mtoto</u> amewekwa rehani kwa aqiqa yake…”

Na kwa hadith;

“Kila <u>mtoto</u> na aqiqa yake…”

Na tamko hili “mtoto” limekusanya kila mtoto hata kama hajakamilisha siku saba ya uhai wake.

Na hii ndio madh-hab ya Hanaabila na Shaafi’iyya, na wakaitilia nguvu qauli hii Sheikh Bin Baaz na Utheimin Allah awarehemu.

Aliulizwa Sheikh Muhammad Bin Swaleh Al-Utheymin -rahimahullah-;

Mtoto aliezaliwa, akafa punde tu alipozaliwa, je atachinjiwa Aqiqa?

Akajibu; "Ndio, pindi anapozaliwa mtoto baada ya kukamilisha miezi minne basi atachinjiwa [Aqiqa] na atapewa jina, kwa sababu baada miezi minne huwa ashatiwa roho na atafufuliwa siku ya qiyama."

[Liqaa'ul baab al-maftuh kaseti nambari (2)].

KIWANGO CHA AQIQA

Sunna kwa mtoto wa kiume ni mbuzi au kondoo wawili na kwa mtoto wa kike ni mbuzi/kondoo mmoja.

Kwa hadith ya Umm Kurz Al-Ka'abiyya asema: Nilimsikia Mtume ﷺ akisema:

"Kwa mtoto wa kiume, mbuzi au kondoo wawili walio sawa, na kwa mtoto wa kike, mbuzi au kondoo mmoja."

Tirmidhi [1516] Nasai [4217] na Irwaa-ul-Ghalil [4/391].

Amesema Al-Imam Nawawy –rahimahullah- ;

"Sunna ni achinjiwe mtoto wa kiume mbuzi au kondoo wawili, na mtoto wa kike mbuzi au kondoo mmoja….."

Sharh Al-Muhadhab [8/409].

Amesema Sheikh Swaleh Al-Fawzan –hafidhahullah-;

“Na hikma ya kutofautisha baina ya mke na mume katika kiwango, ni kwamba [mke] ni nusu ya mwanamume katika Ahkaam, na neema ya mume kwa baba ni yenye kutimia zaidi, na furaha ni kamili zaidi, ikawa kushukuru kwa [kuzaliwa] mume ni zaidi.”

Al-Mulakhas Al-Fiqhy [ukurasa; 215].

Amesema Sheikh Ibn Utheymin –rahimahullah-;

“Asipopata mtu isipokuwa mbuzi au kondoo mmoja (kwa ajili ya mtoto wa kiume), anatosheleza, na atakuwa ametimiza malengo, lakini ikiwa Allah amempa utajiri basi wawili ni bora”

Sharh-ul-Mumti’i [7/492].

Amesema Sheikh Swaleh Al-Fawzaan –hafidhahullah-;

“Lau akichinja mmoja leo na wa pili akamchinja baada ya masiku…hakuna katazo, wala si lazima mbuzi au kondoo wale wawili wakusanyike kwa wakati mmoja”

Al-Muntaqaa min Fatawa Al-Fawzan.

HUKMU YA KUCHINJA MNYAMA MWENGINE MBALI NA MBUZI AU KONDOO

Ametaja Imam Tahawy na Albaihaqy kwamba Ibn Abi Muleika: asema; Abdul Rahman ibn Abi Bakr aliruzukiwa mtoto wa kiume. Aisha -radhiallahu anhaa- akaambiwa [kuwa]: alichinjiwa ngamia,

Akasema [Aisha]: **“Nataka hifadha kwa Allah, Si Mtume amesema mbuzi au kondoo wawili walio sawa.”**

Isnaad yake ni Hassan, [Al-Irwa’a (4/390)].

Na ametaja Ibnul Qayyim Aljawziyya katika Tuhfatul Maudud:

“Kwamba Abu Bakra aliruzukiwa mtoto wa kiume [Abdul Rahman], akamchinjia ngamia, akawalisha watu wa basra. Wengine wakakanusha kitendo [chake] hicho. Wakasema: Mtume ﷺ ameamrisha mbuzi au kondoo wawili kwa mwanamume na mbuzi au kondoo mmoja kwa mtoto wa kike.”

IPI BORA? KUCHINJA AU KUTOA THAMANI YAKE??

Kuchinja ni bora kuliko kutoa sadaqa kwa thamani yake hata ikizidi [hiyo thamani], bali haitoshelezi [thamani] kamwe, kwa sababu, nafsi ya kuchinja na kumwaga damu, ni jambo lenye kukusudiwa, kwani ni ibada iliokusanywa pamoja na swala katika sehemu nyingi kwenye Qura’n, kama alivyosema Allah subhaanahu wata’ala:

“Basi sali na uchinje kwa ajili ya Mola wako Mlezi” [Al-Kawthar: 2].

Na akasema tena;

“Sema: Hakika sala yangu, na kuchinja kwangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Allah, Mola Mlezi wa viumbe vyote.”

[Al-An’aam: 162].

Wanasema wanavyuoni wa **Lajna Daaima**:

“Anachinjiwa mtoto wa kiume mbuzi au kondoo wawili, na mtoto wa kike mbuzi au kondoo mmoja wala haitoshelezi kulipa pesa au mfano wake.”

[11/449].

Pia wakaulizwa [Lajna Daaima]:

Je, yatosheleza [mtu] kununua kilo za nyama [na kuzitoa sadaqa] kwa ajili ya aqiqa au lazima achinje?

Wakajibu: “Haitoshelezi ispokuwa [achinje] mbuzi au kondoo mmoja kwa mtoto wa kike na mbuzi au kondoo wawili kwa mtoto wa kiume.”

[11/440].

JE KUNA DHIKR [UTAJO] MAALUM WAKATI WA KUCHINJA AQIQA?

Amesema Sheikh Muhammad Ali Farkous -hafidhahullah-;

“Kusema Bismillah ni sharti katika kuchinja mnyama ili awe halali, na yule atakae acha kusudi basi si halali kichinjo chake, kwa qauli ya Allah alietukuka “Basi kuleni katika walio somewa jina la Mwenyezi Mungu” [Al-An’am; 118] na kwa qauli yake “Wala msile katika yale wasio somewa jina la Mwenyezi Mungu” [Al-An’am; 121].

Na ni sunna kwa yule mwenye ujuzi, amchinje kwa mkono wake, na amuelekeze kibla na aseme:

“Bismillah Wallahu Akbar, Allahumma hadha minka wa lak, hadhihi aqiqatu fulan ibn fulan”

Na asiposema [hadhihi aqiqa fulan ibn fulan] na akatia nia peke yake basi inamtosheleza in shaa Allah”

[Arbauna Sualan fi Ahkaamil Mauluud].

KUIGAWA NYAMA YA AQIQA

Haikupokewa hadithi yoyote kutoka kwa Mtume ﷺ kuhusu njia maalum ya kuigawa nyama ya Aqiqa, na lengo ni kujikurubisha kwa Allah subhanahu wa ta’ala kwa kumwaga damu, kwa ajili ya kumshukuru Allah kwa neema ya mtoto, na kumkomboa kutokamana na sheitan.

Alikuwa Ibn Siirin akisema:

“Ifanye [nyama ya] aqiqa vile unavyotaka.”

[Tuhfatul Maudud].

Asema **Al-Imam Albany** –rahimahullah-:

‘Wewe uko huru, ukitaka kula [nyama yote] wewe na familia yako, kwa muda wa wiki, na wiki mbili au tatu, na ukitaka itoe sadaka yote, na ukitaka changanya baina ya kula na sadaka, na ukitaka, alika watu, matajiri na mafukara, na bora ya mualiko ni wa mafukara.

Umuhimu [ni kuwa]; Hakuna katika sheria [kwamba] mtu analazimishwa kufanya kitu maalum ispokuwa [kupatikane] kumwaga damu. Kila anaechinja kwa mnasaba wa mtoto aliezaliwa basi ana khiari na kufanya vile anataka.’

HUKMU YA KUVUNJA MIFUPA YA MNYAMA WA AQIQA

Ametaja Imam ibnul Qayyim –rahimahullah- katika kitabu chake **“Tuhfatul Maudud”** kutoka kwa ibn Shihab:

“Hakuna ubaya kuvunja mifupa yake, nayo ni qaul ya Malik, na wale wanaoona [kujuzu] kuvunjwa mifupa yake wanasema: hakujathibiti hadith yoyote sahih inayo kataza jambo hilo wala kuonyesha umakruhu wake, na ada ya watu imeenea katika kuvunja mifupa ya mnyama [aliechinjwa], na katika hilo [kuvunja mifupa] kuna maslaha katika kuliwa kwake na ukamilifu wa kunufaika kwake….”

HUKMU YA KUKUSANYA NIYYAT (MBILI) YA AQIQA PAMOJA NA UDH-HIYA

Aliulizwa Al-Imam Albany –rahimahullah-:

Mtu hakuweza kuwachinjia watoto wake aqiqa, ikaja siku ya Eidul-Adh’ha, akachinja mnyama wa udh’hiya kisha akaingiza ndani yake nia ya aqiqa, je inajuzu?

Akajibu: “Ikiwa wataka nikujibu kwa ufupi basi, haijuzu.

Na ufafanuzi wake unatofautiana kulingana na maoni ya wanavyuoni:

Yule anaeona kwamba aqiqa ni sunna na udh’hiya pia ni sunna……basi atapata thawabu ya udh’hiya pamoja na aqiqa. Hii ni kwa yule anaeona kwamba zote mbili ni sunna.

Ama yule anaeona –mfano wangu- kwamba zote mbili ni wajib, basi wajibu mmoja hautoshelezi mwengine, basi itakuwa ni lazima achinje aqiqa na achinje pia udh’hiya.”

[Silsilatil Hudaa wa Nnur kaseti nambari (689)].

JE INASHURUTISHWA KATIKA AQIQA KAMA VILE INAVYOSHURUTISHWA KATIKA UDH'HIYA?

Kundi la wanavyuoni wameenda na qauli kwamba, inashurutishwa katika aqiqa yale yanayoshurutishwa katika udh'hiya kwa kuzingatia umri [wa yule mnyama], na kutopatikana aibu au ila [kwa yule mnyama], kwa kufanya qiyas ya mnyama wa udh'hiya.

Na wameenda Ibn Hazm na Shaukany kutozingatia masharti hayo, na hii ndio qauli sahihi, kwa kukosekana dalili ya masharti haya [kwa mnyama wa aqiqa].

Lakini wameafikiana kuwa ni bora awe [mnyama yule] mnono na amesalimika kutokamana na aibu/ila.

Amesema mwanachuoni Mubarakfuury –rahimahullah- katika 'Tuhfatul Ahwadhy' (5/96):

"Hakujathibiti masharti [yoyote] katika hadithi sahihi katu, bali wala hadithi dhaifu, na wale wanaoshurutisha masharti hayo basi hawana dalili ispokuwa ni qiyas."

Asema Imam Shaukany –rahimahullah-:

"Na imetolewa dalili kwa kuachiliwa [lafdhi ya] mbuzi/kondoo wawili kwamba, hakuna masharti yoyote [yenye kuzingatiwa], nayo ndio haki, lakini si kwa kuachiliwa [lafdhi hii] bali kwa kukosekana dalili juu ya masharti haya na aibu zilizotajwa katika udh'hiya, na hizi ni hukmu za kisheria hazithibiti isipokuwa kwa dalili. Na haijifichi kwamba italazimu kwa muktadha wa qiyas hiki, kuwa, kila kichinjo kinachokurubishwa kwa Allah subhaanahu wata'ala kiwe na masharti haya, kama vile vichinjo vya walima [vyote vinapendekezwa

kisheria], na vinakurubishwa kwa Allah subhaanahu wata'ala, wala sijui [mwanachuoni yoyote] anaesema kwamba inashurutishwa katika vichinjo vya walima yale yanayoshurutishwa katika udh'hiya, basi hiki qiyas kimelazimu mambo ambayo hawajasema wanavyuoni wowote, na linalolazimu batil basi huwa ni batil [moja kwa moja].

[Neilul Autaar (5/19)].

KUALIKA WATU KWA AJILI YA AQIQA

Asema Al-Imam Albany –rahimahullah-:

"Nimehisi kwamba wengi katika ndugu zetu ambao wanaihuisha sunna hii [ya aqiqa] kana kwamba wanalazimisha kuwe na mualiko, haya madai hayana msingi wowote katika sunna [hivyo basi waweza kualika na kutoalika]."

[Silsilatil Hudaa wa Nnur kaseti nambari (20)].

KUKOPA KWA AJILI YA AQIQA

Kukopa kwa ajili ya Aqiqa kunatofautiana kulingana na hali ya mtu, ikiwa anajua kulingana na hali yake kwamba ataweza kulipa basi itajuzu kwake yeye kukopa, na ikiwa anajua kulingana na hali yake na pato lake kwamba hatoweza kulipa basi ni haramu kwake yeye kukopa kwa sababu atakuwa ni mwenye kula mali za watu kwa batil kwa jina la deni.

Asema Sheikh Muhammad Ali Farkous –hafidhahullah-;

“Jambo hili linatofautiana kulingana na yule alieruzukiwa mtoto, ikiwa ataweza kulilipa lile deni au laa, ikiwa atakuwa na uwezo wa kulipa basi yapendekezwa kwake yeye kukopa kwa ajili ya Aqiqa”

[Arbauna Sualan fi Ahkaamil Maulud].

KUMPA KAFIRI KATIKA NYAMA YA AQIQA

Asema Sheikh Ibn Utheymin rahimahullah:

“Makafiri hupewa katika nyama ya aqiqa ikiwa hawadhuru waislamu….kwa qauli ya Allah alietukuka: “Allah hawakatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Allah huwapenda wafanyao uadilifu.” Yaani, hawakatazi kuwafanyia wema na kuwapa sadaqa. Kwa hivyo hakuna kuzuizi chochote katika kuwafanyia wema na uadilifu…”

Liqaaul Baab Al-Maftuuh [17/35-36].

TOFAUTI BAINA YA UDH’HIYA NA AQIQA

1. Kichinjo cha udh’hiya, inapendekezwa kusema ‘Allahumma taqabbal minni wa min Aal baity’ lakini katika Aqiqa husemwa kama inavyosemwa katika vichinjo vengine “Bismillah Wallahu Akbar”.

2. Mwenye azma ya kuchinja kichinjo cha udh’hiya, hujiepusha na kunyoa nywele zake na kukata kucha zake, kinyume na aqiqa.

3. Yajuzu kushirikiana katika udh-hiya [ikawa ng'ombe/ngamia mmoja ni kwa watu wawili hadi saba] kinyume na aqiqa.

KUMPA MTOTO JINA

WAKATI GANI MTOTO HUPEWA JINA?

Inapendekezwa kumpa mtoto jina siku ya saba ya kuzaliwa kwake, na inafaa kabla yake na baada yake [pia].

Asema Mtume ﷺ :

"Kila mtoto amewekwa rehani kwa aqiqa yake, atachinjiwa siku ya saba na atapewa jina."

Ameisahihisha Albany katika [Al Irwaa (4/394)].

Asema Sheikh Abdul Muhsin Al-Abbad:

"Na kupewa [mtoto] jina siku ya saba, imekuja hadith, lakini pia imekuja [hadith ya kupeana jina kwa mtoto] kabla ya siku ya saba, imekuja katika sahih kwamba Mtume ﷺ asema:

"Nimeruzukiwa usiku mtoto wa kiume nikamuita Ibrahim."

Hii ni dalili kwamba jambo hili [la kupatiana jina] lina ukunjufu, na kwamba yawezekana kumpa mtoto jina siku ya saba na pia yawezekana kabla yake…"

[Sharh Sunan Abi Daud kaseti nambari (209)].

KUMPA MTOTO JINA ZURI

Na yamuajibikia mzazi kumpa mtoto wake jina zuri, kwa hadith ya Abi Dardaa –radhiallahu anhu- asema; Asema Mtume ﷺ :

“Hakika nyinyi mutaitwa siku ya qiyama kwa majina yenu na ya baba zenu, basi yafanyeni mazuri majina yenu.”

Abu Daud [4948], Ibn Hibban [1944], Baihaqy [9/306].

Na akasema Mtume ﷺ katika hadithi ya Ibn Omar –radhiallahu anhumaa-

“Hakika majina yanayopendeza zaidi kwa Allah ni Abdullah na Abdul-Rahman.”Muslim [2132].

Na katika Sunan Abi Daud, asema Mtume ﷺ :

“Itaneni kwa majina ya mitume, na majina yanayopendeza zaidi kwa Allah ni Abdullah na Abdul-Rahman na [majina] yaliyo kweli kabisa ni Harith na Hammam, na yale mabaya zaidi ni Harb na Murra.”

Abu Daud [4950] na akaisahihisha Al-Imam Albany [rahimahullah].

Na wameafikiana wanavyuoni kuwa yanapendekezwa majina yanayo nasibishwa na Allah subhaanahu wa ta’ala kama vile Abdullah, Abdul-Rahman, Abdul-Rahim na mengineo.

Na ni haramu kunasibisha majina ya “Abd” kwa asiekuwa Allah Subhanahu wa ta’ala, kama vile Abdi Omar, na Abdul-Kaaba na Abdul-Hussein na Abdul-Ali…

Amesema Al-Imam Ibn Hazm –rahimahullah-;

“Wameafikiana juu ya uharamu wa kila jina la “Abd” kunasibishwa kwa asiekua Allah….ispokuwa Abdul-Mutalib”

Maraatib-ul-Ijmaa [154].

Na haki ya kutoa jina ni ya baba bila khilaf baina ya wanavyuoni kwa sababu [mtoto] atanasibishwa kwa babake wala sio kwa mtu mwengine yoyote.

KUNYOA NYWELE ZA MTOTO

Sunna ni kunyoa nywele za mtoto siku ya saba, kwa hadith ya Mtume ﷺ inayosema:

“Kila mtoto amewekwa rehani kwa aqiqa yake, atachinjiwa siku ya saba, na <u>ataondolewa udhia [kunyolewa nywele]</u> na atapewa jina.”

Sahih Sunan Abi Daud [2463].

Kama vile ni sunna kutoa sadaka fedha (silver) kwa kiasi cha uzito wa nywele zake, kwa hadith ya mtume ﷺ alipomwambia Fatima alipomzaa Al-Hassan:

“Nyoa nywele zake na utoe sadaka kwa uzito wa nywele zake fedha [silver], kwa maskini.”

Ameipokea Ahmad na akasema Albany katika Al-Irwaa [hadith] ni Hassan [4/402].

Asema Ali bin Abi Talib: **“Tukazipima [nywele zake] tukapata uzito wake ni kiasi cha dirham moja.”**

HUKMU YA KUTOA THAMANI BILA KUNYOA NYWELE WALA KUPIMA

Mtoto asiponyolewa nywele zake, sawa kwa udhru au bila udhru; basi hakuna dhambi, kwa sababu kunyoa nywele ni sunna wala sio wajib, ispokuwa yatakikana afanye bidii kukisia uzito wa nywele zake kisha atoe sadaqa fedha (silver) kwa kiasi cha uzito huo.

Asema Al-Imam Ibn Utheimin –rahimahullah-:

“Kunyoa nywele za mtoto wa kiume siku ya saba ni sunna, …lakini kwa sharti awe yule mwenye kunyoa ni mjuzi, asikijeruhi kichwa [cha mtoto], wala kusipatikane madhara kwa mtoto. Akikosekana [kinyozi mzuri] basi naona asinyolewe na itolewe sadaka fedha [silver] kwa kiwango cha nywele zake [kwa kukisia].”

Liqaaul Baab Al-Maftuuh [120].

FAIDA YA KUNYOA NYWELE ZA MTOTO

Asema Mtume ﷺ :

“Kila mtoto amewekwa rehani kwa aqiqa yake, atachinjiwa siku ya saba, na <u>ataondolewa udhia</u> [kunyolewa nywele] na atapewa jina.”

[Sahih Sunan Abi Daud (2463)].

Asema ibnul Qayyim – rahimahullah-:

“Na ikawa kunyoa nywele ni <u>kumuondolea udhia</u> [mtoto yule], na <u>kuzitoa nywele dhaifu ili zije baada yake nywele zilizo na nguvu zaidi na zenye manufaa zaidi kwa kichwa</u>…”

[Tuhfatul Maudud fi Ahkaamil Mauluud].

KUNYOA NYWELE ZA MTOTO WA KIKE

Wametofautiana wanavyuoni juu ya mas'ala haya, lakini kauli sahihi [na Allah ajua zaidi] ni kuwa mtoto wa kike ananyolewa kama vile mtoto wa kiume wala hakuna tofauti yoyote.

Asema Al-Imam Assan'aany –rahimahullah- katika Subul Salam:

"Qauli yake [Mtume ﷺ] katika hadithi ya Samura: "Na hunyolewa": Ni dalili ya kunyolewa kwa mtoto siku ya saba, na dhahir yake ni kuwa <u>imekusanya mtoto wa kiume na wa kike</u>.'

Aliulizwa Sheikh Albany –rahimahullah-:

"Je mtoto wa kike hunyolewa nywele zake anapozaliwa?

Akajibu: "[Ananyolewa] <u>Kama mtoto wa kiume</u>."

[Silsilatil Hudaa wa Nnur kaseti nambari (564)].

HUKMU YA ADHANA NA IQAMA KWENYE SIKIO LA MTOTO

Haijathibiti hadithi yoyote sahih kutoka kwa Mtume ﷺ juu ya haya,na hadithi iliokuja ni dhaifu, katika isnad yake yupo Aasim ibn Ubeidillah ibn Aasim ibn Omar nae ni dhaifu.

Wala haikuhifadhiwa kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba aliadhini au kukimu kwenye sikio la mwanae Ibrahim pindi alipozaliwa, vile vile watoto waliokuwa wakiletwa kwake kwa ajili ya kuwafanyia Tahnik na kuwapa majina…haikupokelewa kwamba alikuwa akiadhini au akikimu.

Asema Sheikh Khalid Al-Musheiqih –hafidhahullah-;

"Hukmu ya Adhan na Iqama katika sikio la mtoto aliezaliwa <u>si sunna</u> kwa sababu iliokuja ni hadithi dhaifu, haikuthibiti kutoka kwa Mtume ﷺ "

TAHNIK

Tahnik: Ni kule kutafuna tende hadi ilainike kisha kuiweka kwenye mdomo wa mtoto aliezaliwa na kuisugua kwenye mafizi yake.

amepokea Abu Musa -radhiallahu anhu- asema:

“Niliruzukiwa mtoto wa kiume, nikampeleka kwa Mtume ﷺ akamuita Ibrahim kisha akamsugua mafizi yake kwa tende.”

Bukhari [5045].

Imekuja katika fatawa za wanavyuoni wa **Lajna Daaima**, wanasema:

“Kumfanyia tahnik mtoto aliezaliwa ni sunna iliothibiti kwa kitendo cha Mtume ﷺ kwa haki ya watoto wa baadhi ya masahaba – radhiallahu anhum- , na hii yaonyesha kuwa hukmu hii imeenea [pia] kwa umma wake, kwa qauli ya Allah alietukuka:

“Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Allah…”

[Ahzaab: 21].

Ama wakati wa Tahnik ni punde tu anapozaliwa….

Imekuja katika sahih Bukhari na Muslim kutoka kwa Anas bin Malik – radhiallahu anhu- asema:

“Nilimpeleka Abdullah bin Abi Talha kwa Mtume ﷺ pindi alipozaliwa…Akaniuliza: “Je, una [umebeba pamoja na wewe] tende?”

Nikamjibu: “Ndio, nikampa baadhi ya tende, akazitia [Mtume sallallahu aleihi wasallam] kwenye mdomo wake na kuzitafuna kisha

akazitia kwenye mdomo wake [yule mtoto]….kisha akamuita [akampa jina la] Abdullah.”

Bukhari [5470], Muslim [2144].

Aliulizwa Sheikh Abdul muhsin Al-Abbad –hafidhahullah-:

Je, tahnik inakuwa punde tu baada ya kuzaliwa mtoto?

Akajibu: “Ndio, inakuwa punde tu baada ya kuzaliwa mtoto.”

[Sharh Sunan Tirmidhy kaseti nambari (414)].

Na asli katika tahnik, ni kutumia tende, lakini inafaa kutumia vitamu vyengine kama asali na mfano wake, kwa sababu lengo ni kuingiza kitu kitamu kwenye tumbo la yule mtoto.

Asema mwanachuoni **Abdul-Muhsin Al-Abbad** –hafidhahullah-:

“Kwanza [tahnik], si kwa ajili ya tabarruk [kutaka Baraka] bali iwe kitu cha kwanza kuingia kwenye tumbo la mtoto ni kitu kitamu, <u>hili ndilo lengo, kupatikane utamu.</u>’

[Sharh Sunan Tirmidhi kaseti nambari (414)].

والله أعلم

سبحانك اللهم وبحمدك أشهد أن لا اله الا أنت أستغفرك وأتوب اليك